# UANAFUNZI UNAOBEBA MAONO NA MKAKATI

## KITABU CHA KUJIFUNZIA

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Amina. (Mathayo 28: 19-20)

FDM .WORLD

Craig Caster

*Discipleship Takes Vision and Strategy* in Swahili

HUDUMA YA UANAFUNZI KATIKA
FAMILIA

(619) 590-1901
info@FDM.world
www.FDM.world

Uanafunzi Unaobeba Maono na Mikakati: Craig Caster
ISBN 978-1-7334130-6-0
Ili kuprinti au kupata maunzi laini ya chapisho hili; hakimiliki kwa Craig Caster ©2022- 04192022 (kuchapishwa tena).

Nukuu zote za Maaandiko Matakatifu katika tafsiri hii zimetolewe katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV); isipokuwa pale itakapotafsiriwa vinginevyo kama ilivyo katika nakala ya awali (nakala ya Kiingereza). Hatimiliki © Chama cha Biblia cha Kenya na Chama cha Biblia cha Tanzania (1997), Maandiko yote yametumika kwa ruhusa maalumu na haki zote zimehifadhiwa.

Pasipo ukomo wowote, si ruhusa kunakili, kuchapa au kuandika upya chapisho hili au sehemu ya chapisho (kwa mfumo wa e-book) au namna nyingine yoyote inayoweza kutengenezwa, kutunzwa au kutambulishwa kwenye mfumo wa upatikanaji tena, au kusambazwa; kwa umbo au kwa namna yoyote (kielektroniki, mekanikia, fotokopi, kurekodi, au vinginevyo), bila ruhusa toka katika hatimiliki zilitajwa hapo juu.

**Matini nyingine za Kujifunzia kutoka FDM.world**

*Christian Foundational Truths: A Strong Foundation for a Disciple by Craig C aster*

*Forgiveness and Reconciliation by Craig Caster*

*Marriage Is a Ministry series by Craig Caster*

*Parenting Is a Ministry series by Craig Caster*

*Understanding Teens series by Craig Caster*

Vitabu vyote vya kujifunzia kutoka FDM.world vinapendekezwa kwa matumizi ya masomo binafsi, katika vikundi vidogo vidogo kama nyezo za kujifunzia, pamoja na kutolea ushauri na saha.

# YALIYOMO


Utangulizi…………………………………………………………………………………....1

Uanafunzi wa Leo………………………………………………..…………………..2

Kupanga Vipaumbele Vinavyohusiana…………………………………………….…...5

Kuuelewa Uanafunzi wa Kweli……………………………………………………………8

Kuiga Mfano wa Kristo……………………………………………………………..13

Fanya kila Kiongozi awe Mwanafunzi……………………………………………..15

Fanya kila Muumini awe Mwanafunzi ……………………………………………….19

Kuanza…………………………………………………………………………………...24

Wito wa Kutenda…………………………………………………………….........25

Kuhusu Mwandishi…………………………………………………………………28

Kuhusu Huduma ya Uanafunzi katika Familia (FDM)……………………….................29

## UTANGULIZI

Uanafunzi ni kiini cha shauku ya Mungu kwa watu wake. Tunatambuaje hili? Kitabu cha Mathayo kinaliandika suala la kufanya watu kuwa wanafunzi kama maagizo ya mwisho ya Yesu aliyotoa kwa mitume wake kabla ya kupaa kwenda Mbinguni.

> Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa Dahari. (Mathayo 28:19-20)

Huduma ya Uanafunzi katika Familia (FDM) inalipa uzito agizo hili na imekuwa ikiandaa wachungaji na walei kwa miaka mingi sasa. Lengo letu kwenye kijitabu hiki ni kusaidia wachungaji kupata maono ya Uanafunzi na kuandaa mikakati inayolilenga kundi fulani la waamini wao. Hatimaye, kuwasaidia Wakristo kukua kiimani na kujifunza kuwafanya wengine kuwa wanafunzi wa Yesu katika harakati ya kutimiza Utume Mkuu.(Agizo kuu)

Matini hii inabeba mtazamo wa Kibiblia juu ya umuhimu mkubwa na uhitaji wake katika mkakati wa kufanikisha kuwapo kwa Uanafunzi. Tunaelewa matatizo yanayowakabili viongozi wa makanisa juu ya vuguvugu la utamaduni wa Kikristo; na kwamba inaweza kuwa ngumu kwa wao kuamua ni mikakati ipi ya Uanafunzi ipewe kipaumbele na kutumika ndani ya makanisa yao husika. Mara nyingi, viongozi wa makanisa wanashindwa kujua ikiwa mafundisho yanayotolewa madhabahuni yanatosha au pengine suluhisho ni kuanzisha huduma za ziada na vikundi vya majumbani ambavyo huongozwa na walezi wasio na mafundisho yoyote. Ili kufanikisha kuwepo kwa Uanafunzi, lazima pawepo na maono dhahiri, mikakati na mpango wa namna ambayo si tu kwamba utatambulisha waamini ndani ya kanisa lako, bali utaongeza idadi ya waamini pia. Hii ndiyo maana halisi ya Utume Mkuu yaani, kuutambulisha na kuukuza Ufalme wa Mungu.

Maombi yetu ni kwamba, kijitabu hiki kiwasilishe mtazamo wa Mungu katika umuhimu mkubwa wa uanafunzi na hitaji la kutekelezwa kwa maono na mikakati dhahiri kwa ajili ya kanisa lako; kwanza kwa viongozi, na kisha kwa kundi lako. Tunaomba pia kwamba, shauku ya Mungu kwa uanafunzi wa kweli iwe ndiyo maono ya kanisa lako na msukumo wa kuendelea mbele zaidi. Mungu abariki mipango na jitihada zako.

## UANAFUNZI WA LEO

Kabla Bwana Yesu hajapaa mbinguni, aliwaagiza mitume kuwafanya watu kuwa wanafunzi na kuwafundisha watakatifu kuyashika yale yote yaliyojumuishwa katika Neno la Mungu. Utaratibu huu ulidhihirishwa kwa mara ya kwanza na Yesu mwenyewe katika huduma yake kwa makusanyiko, na kisha wafuasi wake katika kuunda Kanisa la kwanza. Kama Wakristo, nasi sasa tunapewa agizo hilihili la kuwafanya watu kuwa wanafunzi na kuwafundisha kujua Mungu ni nani na jinsi ya kuishi kwa ajili yake. Ni amri ambayo anawapa waamini wote kuifuata mpaka mwisho wa nyakati, kwa kuwa ndiyo utume wetu tukiwa hapa duniani. Lakini kwa sasa ni makanisa mangapi yanaendeshwa kwa ufahamu kamili wa amri ya Yesu? Cha kusikitisha ni kwamba, sio mengi. Nini kinaendelea? Nini au nani wa kulaumiwa? Uongozi wa kanisa unaweza kuwalaumu waamini kwa uvivu wao au hata kwa wao kutokuwa tayari kutii mapenzi ya Mungu nyakati wanapokabiliwa na vishawishi na masumbufu ya ulimwengu tunamoishi. Lakini tatizo halisi sio uvivu mkubwa au kile kinachotokea nje ya makanisa na nje ya familia zetu, bali ni kile tusichokifanya ndani ya makanisa na kwenye familia zetu.

Tumeyagawanya matatizo ya uanafunzi wa leo katika makundi makubwa matatu:

1. Kukosekana kwa uelewa juu ya mpango wa kipaumbele cha Mungu kwenye mahusiano yetu
2. Kukosekana kwa uelewa juu ya Uanafunzi wa kweli
3. Kukosekana kwa kusudio thabiti katika makanisa na kwenye familia zetu

### Kukosekana kwa Uelewa juu ya Mpango wa Kipaumbele cha Mungu kwenye Mahusiano yetu

Makanisa ya Kiinjili yanakumbatia sura ya 28:19-20 ya Kitabu cha Mathayo, kama Agizo Kuu la Yesu katika kutafuta na kuokoa watu kwa njia ya kuihubiri Injili. Lakini hali ya kiroho ya wengi wanaojiita waamini na kwamba wako ndani ya Kristo pamoja na familia zao inasikitisha; kwa kuwa ukweli ulio wazi ni kwamba, Wakristo wachache tu ndio wamefundishwa ipasavyo. Hawajui jinsi ya kuzingatia mambo ambayo Mungu amewapa kwa kufuata mpangilio wa vipaumbele vyake; ambayo ni, "kushika yote niliyowaamuru" ili waweze kuhusiana vyema na Mungu, wenzi wao, watoto, pamoja na watu wengine maishani mwao.

Leo hii, Wakristo wengi hawaenendi katika nguvu za Mungu kwa sababu hawajui umuhimu au ulazima wa kukaa ndani ya Yesu kila siku (Yohana 13:7). Kwa sababu ya hii, familia za Kikristo zinavuna matunda mabaya ya uzembe huu. Haya yanajidhihirisha katika viwango vikubwa vya talaka kwa Wakristo ikilinganishwa na viwango vya talaka kwa wasio Wakristo; tunaweza kuyaona hayo kwa watoto wetu pia. Watoto wengi kutoka familia za Kikristo wamekuwa waathirika wa dawa za kulevya, ulevi wa kupindukia, pamoja na kujihusisha na dhambi ya ngono na mahusiano yasiyofaa. Uasi na ukosefu wa heshima kwa wazazi pamoja na mamlaka, kwa sasa vinachukuliwa kama tabia za kawaida za ujana hata katika Kanisa. Ukweli ni kwamba, Wakristo wengi ni wadhaifu kiroho na familia zetu zina janga kubwa.

Hapo mwanzo, baada ya Mungu kumuumba Adamu na Hawa, aliunda familia. Ni wazi kwamba familia ni muhimu kwake na inapaswa kupewa kipaumbele katika mkakati wa kanisa wa kufanya watu kuwa wanafunzi. Leo hii, familia nyingi kanisani zinashindwa; kwa kuwa hawana tena maarifa waliyopewa na Mungu ili yawasaidie kujenga na kudumisha familia bora. Makanisa hayapuuzi janga hili kwa makusudi, bali yanakosa maono ya muundo bora wa huduma ya uanafunzi katika familia na hayajandaa mikakati ya Kibiblia ili kuwawezesha

waamini kufikia mafanikio. Mungu anauchukulia utunzaji wa familia zetu kuwa ni muhimu zaidi kuliko kazi, mapendeleo yetu, au hata kuhudumu kanisani. Lakini waamini wengi hawaishi namna hii na hawajawahi kufundishwa ukweli wa Kibiblia ambao unatumika katika maisha ya familia. Asasi ya familia ndio msingi wa mafunzo ya huduma kwa waume na wake, na Mungu anatutaka tujue na kufuata maagizo ya Kibiblia aliyotupa juu ya jinsi gani kutimiza majukumu haya muhimu. Kila kitu huanzia katika familia. Hapa ndipo pa kuanzia.

**Kukosekana kwa Uelewa juu ya Uanafunzi wa kweli**

Ikiwa utawauliza Wakristo wa kawaida kufafanua maana ya uanafunzi, wangeweza kusema kuwa; ni kuwaanzishia masomo waamini wapya ambapo hujifunza mafundisho ya msingi wa Imani. Kwa hakika hili ndilo jambo umuhimu zaidi, ingawa kuna mengine zaidi ya hayo. Kufundishwa maana yake ni kujifunza jinsi ya kuwa kama Yesu yaani, jinsi ya kutenda kwa usahihi kila kitu alichotuamuru tufanye kwa neema yake. Matarajio ni kwamba, mwanafunzi atakapokomaa kiimani ataanza kuwafundisha wengine.

Katika Kitabu cha Mathayo 28:19-20, Yesu anaweka wazi kusudi kuu na la msingi kwa Kanisa kuwa, “Utume Mkuu.” Kutokana na ukweli huu, lazima tuzingatie swali hili muhimu; ikiwa kufanya watu kuwa wanafunzi kunastahili kuwa kusudi kuu na la kipaumbele kwa Kanisa, kwa nini waamini wengi wa leo hawajui maana ya mwanafunzi na uanafunzi? Na ikiwa wanafahamu, kwa nini hawajaitika wito na kuwa wanafunzi?

Utii wa Bwana wetu ulikuwa kwa mapenzi kamili ya Baba yake. Aina ya leo ya Utume Mkuu wa Yesu inaelekeza tu kwamba ni, “Lazima tufanye kazi! Wapagani wanakufa bila kumjua Kristo; lazima twende tukawaambia habari zake.” Hii ni kweli kabisa, lakini vipi kuhusu yale mambo mengine yaliyopo katika mstari wa 19 na 20 yaani, vipi kuhusu “mafundisho?” Lazima tufanye kazi na Mungu kwa kutii mapenzi yake kamili kwetu sisi kama waamini na wafuasi wa Kristo; kwa kuwa wanafunzi wa Neno Lake, kukua kiimani kila siku na kujichunguza ili kuona kama “vipaumbele” vya Mungu vinatekelezwa ndani yetu wenyewe na katika uhusiano wetu na Yeye. Tukimwamini Mungu katika kutimiza mahitaji yetu na ikiwa vipaumbele vyetu vitaenda sawa na mapenzi yake, atatufungulia milango ya kuwafundisha wengine. Hii ndiyo maana halisi ya katika kiini cha Utume Mkuu wa Kristo.

**Kukosekana kwa kusudio thabiti katika makanisa na kwenye familia zetu**

Uanafunzi sio hiari. Makanisa yote na waamini lazima waelewe kuwa tumepewa jukumu hili la uanafunzi, wito kamili toka kwa Mungu, lakini hawafanyi hivyo; kwa nini? Hii ni kwa

sababu hawaelewi lengo halisi na asili ya mchakato huu wa “kufundisha.” Yesu anatuambia kile kilichopo katika kifungu cha Mathayo 28, tazama:

> Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari (28:19-20).

Awali Maandiko haya yaliandikwa kwa Kiyunani na yako mahususi kabisa. “Fanya wanafunzi” ni tafsiri ya kitenzi ‘fanya’na sentensi iliyobaki inakamilisha kitendo hiki. “Nenda,” “kubatiza,” na “kufundisha” vyote hurejelea kufanya watu kuwa wanafunzi. Pia, msisitizo mkubwa wa amri hii ya Yesu ni kitenzi kikuu, maana yake ikiwa ni kutoa agizo au amri, ambayo huonyesha kuwa ufundishaji huu ni “kutenda na kuendelea kutenda.” Hivyo, Mungu anatuamuru au kutuelekeza kwamba tuwe na uanafunzi endelevu. Kila muumini katika kila Kanisa wakati wote amepewa jukumu hili; kwenda, kubatiza na kufundisha; lakini kwa kawaida haifanyiki hivyo kwa sasa.

Kwa ujumla tunachokiona kwa sasa ni kwamba, Maandiko haya yanafundishwa kwa lengo la kushirikishana Injili ya wokovu na kuwahimiza watu kuzingatia utume huu kama eneo la huduma ya Kikristo. Makanisa na bodi za utume vinawasaidia waamini wanapokusudia "kwenda" kwa mataifa kushirikisha habari hii njema kwa wale wanaoangamia dhambini, na hiki ni kitu kizuri! Lakini kuna ukweli mwingine muhimu unaodhihirishwa pia katika kifungu hiki, ukweli ambao umepotea miongoni mwa waamini na makanisa ya leo. Tunao watu hivi sasa ambao wanapambana ndani ya makanisa na kwenye familia zetu ambao huitaji huduma hii pia. Amri hii ya Yesu inawahusisha pia wale walio katika maeneo yetu ya nyumbani ambayo yana ushawishi, sio tu kwa nchi za mbali.

Tatizo hili ni kubwa na nzito; ndio sababu FDM imeanzisha mchakato wa kuwafanya watu kuwa Wanafunzi wa Yesu, mchakato ambao hujikita katika kushughulikia masuala haya. Acha tukuonyeshe jinsi unavyoweza kuufanya Utume Mkuu kuzaa matunda katika makanisa na kwenye familia zetu.

## KUPANGA VIPAUMBELE VINAVYOHUSIANA

Kwa sababu tunaamini kuwa mafunzo haya ya uanafuzni ni muhimu kwa ukuaji ambao Mungu anataka kuuona kwa watoto wake, tumeandaa matini kama hii kadiri Mungu alivyotuongoza. Ikiwa hauna kitabu kizuri cha kujifunzia uanafunzi wa Kibiblia katika kanisa lako, kinachoelezea misingi ya imani, tunatoa kitabu cha kuanzia kinachoitwa *Christian Foundational Truts: A Strong Foundation for Discipl*e, ambacho kinapatikana kwenye tovuti yetu bure (www.FDM.world au www.discipleshipworkbooks.com).

Njia tatu za FDM katika kuufanikisha uanafunzi wa kweli:

Sehemu ya 1: Kupanga Vipaumbele Vinavyohusiana

Sehemu ya 2: Kuelewa Uanafunzi wa Kweli

Sehemu ya 3: Kuiga Mfano wa Kristo kupitia Uhusiano Mahsusi:

Fanya Kila Kiongozi awe Mwanafunzi

Fanya Kila Muumini awe Mwanafunzi

**Kupanga Vipaumbele Vyetu**

Moja kati ya faida za msingi za uanafunzi wa kweli ni jinsi ambavyo huwafanya waamini kushikamana na kila mmoja kuwajibika kwa mwenzake, jambo ambalo linalandana na mafundisho ya Maandiko. Mungu hataki tu tusikie Neno, bali anatuagiza pia tutafute kujua Maandiko ili tuwe tayari kusaidia wengine kwenye safari yao ya imani. Mungu pia anatuambia tukiri dhambi zetu kwa kila mmoja wetu, tuombeane na tusaidiane katika maisha haya kama Wakristo, wafuasi wa Kristo. Ili kulifanya hili vizuri inahitaji uhusiano wa kibinafsi unaokuzwa na ushirika au kukutana mara kwa mara. Kuna njia nzuri ya kuhusiana, kwa kuwa sio watu wote katika maisha yetu wana uzito au kipaumbele sawa; lazima tupange vipaumbele vya mahusiano yetu kwa kuzingatia mapenzi ya Mungu. Bibilia iko wazi kabisa kuhusu nani anapaswa kupewa kipaumbele kuliko wengine, wa kwanza akiwa ni Mungu.

Watu wengi hutumia miaka mingi vyuoni, kusoma na kupewa ushauri kwa ajili ya wito; Wanatafuta njia za kuwa bora ili waweze kupandishwa vyeo na kupata kazi zenye manufaa zaidi. Tunafanya mazoezi ili tuwe bora kwenye michezo, vitu tunavyovipenda pamoja na kufahamu masuala mengi muhimu ili kulinda afya zetu za kimwili. Lakini tunatumia muda na bidii gani kumjua Mungu ambaye alituumba; yaani, Yeye ambaye ana mamlaka katika maisha ya kila kiumbe hapa Ulimwenguni?

Kama wanafunzi wa Kristo, tunahitaji kuelewa mpangilio sahihi wa vipaumbele vya uhusiano wetu, na pia tunahitaji kujifunza kuyatenda mambo hayo kwa haki. "Kutenda" maana yake ni kutunza au kusimamia kitu au mtu kulingana na mahitaji, kusudi, na kipaumbele chake. Kuwa mwanafunzi wa Neno la Mungu ni pamoja na kujifunza jinsi ya kutenda kwa usahihi majukumu yote ambayo Mungu ametupa. Hivyo je, ni watu gani muhimu zaidi ambao Mungu amewapa waamini kuwatendea haya? Je! Ni upi mpangilio sahihi wa vipaumbele vya mahusiano yetu? Na tulitazame hii sasa.

*Kipaumbele chetu cha kwanza katika mahusiano ni uhusiano tulio nao na Mungu.* Tunaimarisha uhusiano huu kwa kushirikiana naye kila siku, kudumu ndani yake na kujitolea muda kwa ajili

yake. Baada ya Yesu kufa, pazia la hekalu liliraruliwa kutoka juu hadi chini, ikiashiria kuwa utengano kati ya Mungu na mwanadamu ulikuwa umeondolewa. Mtu anaweza kupata ushirika wa moja kwa moja na Mungu, ila tu kwa njia ya msamaha uliopatikana kwa kifo cha Kristo (Mat 27: 50-51). Hii inamaanisha kwamba tunaweza kumwendea Mungu sisi wenyewe, kama mtoto anavyomwendea baba yake.

Katika Kitabu cha Yohana sura ya 17, Yesu aliwaombea wanafunzi wake ili waweze kuwa na *uhusiano wa karibu na Mungu* kama ule aliokuwa nao yeye na Baba yake. Lugha inayoumika hapo inaonyesha kwamba sisi, kama watoto wake, tunaweza kumwita kama "Baba," *na tunaweza kumjia kama mtoto anayetambaa hadi kwenye mapaja ya baba kwa faraja, ushirika, na upendo.* Wakristo wanaweza kufanya hivyo kwa kujifunza kanuni zifuatazo:

- Umuhimu wa kutenga muda wa kuwa na Mungu kwa kila siku.
- Kuzungumza na Mungu, kutoa shukrani, kumsifu na kuomba msaada wake.

- Kusoma Neno lake kwa lengo la kupokea mafundisho na ushirika toka kwake.
- Kufanya tafakari juu ya kile kinachosomwa na hata kufikiria wazo la kuyaweka katika maandishi ili tuweze kukazia akilini mwetu mawazo yanayofundishwa.

Yohana 15:7 inatuambia, “Ninyi mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote, nanyi mtatendewa.” Kukaa ndani ya Mungu ni muhimu kwa maisha ya Kikristo yenye mafanikio. Hii inamaanisha “kukaa ndani yake daima; kuwa na uhusiano wa karibu na wenye kumtegemea yeye.” Endapo Wakristo watafanya hivi, Mungu anawaahidia kuzaa *matunda mengi*! Watakua kiroho, kama vile matunda huonekanavyo kwenye mzabibu. Yohana 15:5 inasema, “Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.” Yesu ndiye mzabibu, na sisi ni matawi. Je! Matunda yanaweza kukua tofauti na mzabibu? Andiko hili linasema, "bila Mimi [Yesu], humuwezi kufanya lolote." Je! Tunaweza kukua kiroho kiasi gani bila Yeye? Hatuwezi kuzalisha chochote peke yetu. Tunategemea kabisa Roho Mtakatifu wa Mungu, Neno Lake, na nguvu Zake. Lazima tujifunze na kukaa ndani ya Kristo ikiwa tunataka kutekeleza majukumu yetu tuliyopewa na Mungu.

*Ikiwa tumeoa, wenzi wetu wana kipaumbele cha pili juu ya mahusiano yote baada ya Mungu.* Ni wazi kabisa katika Maandiko kwamba ndoa ni kipaumbele kwa Mungu, lakini wenzi wengi wa Kikristo hawajui juu ya kutendeana kulingana na Neno la Mungu. Kiwango cha talaka ndani ya Kanisa ni ushahidi tosha wa ukweli huu. Waefeso 5 inazungumza vyema juu ya jinsi waume na wake wanavyopaswa kuhusika ikiwa wanataka kuwa na ndoa yenye mafanikio.

> Enyi wake, watiini waume zenu, kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni Mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. (Waefeso 5: 22-24)

> Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake. (Waefeso 5:25)

*Watoto ni kipaumbele kinachofuata baada ya Mungu na mwenzi.* Kuhudumia familia zetu ni jambo muhimu sana kwa Mungu, kwa maana Mungu anajua familia imara ndio msingi wa jamii. Wazazi wengi huwapa watoto wao kipaumbele zaidi kuliko wenzi wao, utaratibu ambao ni mbaya katika vipaumbele. Bila ndoa imara, familia iko katika machafuko. Kama kichwa cha familia, Mungu amewaelekeza akina baba kuwafundisha watoto katika njia za Bwana (Waefeso 6: 4). Kwa miaka mingi nimekuwa nikizungumza na vikundi vingi vya wanaume, nimekuwa nikiwauliza maswali yafuatayo kujua ni kwa namna gani tumekuwa tukitimiza mapenzi ya Mungu katika utunzaji wa familia zetu:

- Ni wanaume wangapi wamekuwa wakifanya kazi kwa zaidi ya miaka kumi? Ni wangapi walienda shuleni au walipata mafunzo ya kufanya kazi hiyo? (Wengi huinua mikono kujibu).
- Ni wangapi huwa na ujasiri wa kufundisha mwanaume mwingine kufanya kazi kama zao? (Tena, wengi huinua mikono).
- Ni wangapi wameoa kwa zaidi ya miaka kumi? (kwa kawaida, zaidi ya asilimia 75 huinua mikono).
- Ni wangapi wamekuwa na ujasiri wa kufundisha mwanaume mwingine jinsi ya kuwa waume au wazazi bora kulingana na Neno la Mungu? (Mara nyingi, hakuna mkono hata mmoja huinuliwa).

Kwa ufupi, huwa nauliza swali jingine tena; "Je, unafikiri Bwana anajali zaidi juu ya ustadi wako kazini, au juu ya jinsi unavyomtunza mke wako, ambaye ni mmoja wa binti zake?" Siku moja sote tutatoa hesabu ya jinsi tulivyotunza majukumu ambayo Mungu ametupa.

Kuwasaidia viongozi wako na watu katika kusanyiko kuelewa mpangilio sahihi wa vipaumbele vya mahusiano yao ni hatua ya kwanza ya uanafunzi. Kwa nini? Kwa sababu bila mafundisho thabiti ya utaratibu wa vipaumbele vya uhusiano, watu watatumia nguvu na wakati mwingi kwa vitu ambavyo si vya muhimu sana ikilinganishwa na vile ambavyo Mungu anasema ni vya muhimu. Ikiwa tutalielewa hili vizuri, mambo mengine yote maisha yetu yatakuwa sawasawa. Kwa wengi wetu, hiki ni kitu kigumu; lakini acha nikutie moyo kwa Neno hii:

> Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwishakuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu (Wafilipi 3:12).

Mafunzo haya hayatakiwi kumchanganya mtu yeyote, kwa sababu hakuna hata mmoja wetu anayeweza kuwa mkamilifu. Lakini Paulo anasema hivi katika mstari huo hapo juu, "endelea," maana yake ikiwa ni kuyatunza mapenzi ya Mungu mioyoni mwetu na kuyatumia kwa ajili ya maisha yetu ya baadae. Sote tunapaswa kuendelee kujifunza na kushughulika na yale ambayo Mungu anatuambia tufanye kulingana na Neno Lake. Mwanafunzi ni mfuasi wa kujitolea wa bwana wake, mwenye shauku ya kuwa kama bwana huyo. Kwa Wakristo, lengo ni kuwa kama Kristo zaidi.

## KUUELEWA UANAFUNZI WA KWELI

Sehemu ya pili ya mpango wa uanafunzi ni kuuelewa uanafunzi wa kweli. Ni muhimu kuwafundisha viongozi na waamini katika Kanisa juu ya ufuasi gani ni kweli kutimiza Agizo kuu la Mathayo 28: 19-20.

Kanisa ni dhaifu sana katika eneo la kutimiza hili Agizo Kuu kwa watu wetu wenyewe kuliko kushirikishana nao ujumbe wa Injili. Inahitaji mafundisho na maelekezo pamoja na maandalizi ili kujua na kutii Neno la Mungu. Ikumbukwe kwamba mtu anaweza kuwa mwanafunzi baada tu ya kutoa maisha yake kwa Kristo; Mathayo 28: 19-20 inatilia mkazo katika kuandaa watakatifu. Hao ndio walengwa wetu yaani, watakatifu. Acha tuangalie ufafanuzi ufuatao kwa neno mwanafunzi.

> *Mwanafunzi*: (nomino, kwa Kigiriki) "Mathetes" ni mwanafunzi, mtu anayejifunza, au anayetafuta maarifa, lakini ina maana zaidi ya hizo katika Agano Jipya. Ni mfuasi anayekubali mafundisho yote aliyopewa na kuyafanya kuwa kanuni katika mwenendo wake. Katika Kiyunani cha Jadi, "mathetes" ndio ambayo tungeweza kuiita "mwanafunzi," ambaye hajifunza tu ukweli kutoka kwa mwalimu wake bali hujifunza pia mambo mengine kama mitazamo na falsafa zake. Kwa njia hii, "mathetes" ndio tunaweza kumuita "mwanafunzi-mwenza," ambaye siyo tu hukaa darasani kusikiliza mihadhara, bali pia humfuata mwalimu ili kujifunza maisha, ukweli na huendelea kuiga tabia na matendo mema ya mwalimu.

Kwa kifupi, mwanafunzi ni mtu anayejifunza, atafutaye maarifa na ambaye lengo lake ni kufanana na mwalimu wake kitabia. Hivyo basi, mwanafunzi wa Kristo, ni yule anayejaribu kuwa kama Kristo zaidi katika mitazamo, tabia, falsafa, maoni, na matendo yake. Neno "mwanafunzi" limetajwa mara 269 katika Agano Jipya, ambalo linaelezea mwanafunzi wa Kikristo kwa njia nne tofauti:

1. ***Mwanafunzi* amempokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi.**

    Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake. (Yohana 1:12)

Kulingana na Maandiko, mwanafunzi ni mfuasi wa Yesu anayeamini na aliyejitolea. Mwanafunzi anayefaa lazima kwanza atambue kuwa wao ni wenye dhambi chini ya hukumu ya Mungu (Warumi 3:23; 6:23); wanahitaji kukiri dhambi zao kwa Mungu (1 Yohana 1: 9); lazima watubu au waache dhambi zao (Mathayo 3: 2, 8; 4:17; Matendo 2:38); na wanaamini kwamba kifo cha Yesu msalabani kilikuwa malipo ya dhambi zao. Kama kweli mtu anamwamini Yesu, kwamba alisulubiwa kwa dhambi zao, akazikwa, na kufufuka kutoka kwa wafu kama vile Biblia inavyoelezea, basi hurejeshwa katika uhusiano na Mungu na kupewa uzima wa milele mbele Yake (Warumi 10: 9–9). 10; 2 Wakorintho 5:21; 1 Yohana 2: 1-2). Wakati wa wokovu, Roho Mtakatifu huingia ndani ya mtu na Biblia inalielezea hii kama kuwa na uwezo wa Kristo ndani (Matendo 2:38). Hakuna mtu anayeweza kuwa mwanafunzi wa kweli na mtoto wa Mungu bila wokovu kulingana na mpango wa Mungu. Hii ni muhimu kabla ya kuendelea kufundisha au kuwa mwanafunzi kwa sababu Biblia inasema kwamba "asili" au mtu ambaye hajaokoka hawezi kuyaelewa mambo ya Mungu (1 Wakorintho 1:14, 18).

2. *Mwanafunzi* ni mtu anayejifunza Neno.

    Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali nano la kweli. (2 Timotheo 2:15)

Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli. (Yohana 8:31)

Kwa maneno mengine, mwanafunzi hutenga muda wake wa thamani ili kujifunza mapenzi ya Mungu kwa kila nyanja ya maisha. Ni mapenzi ya Mungu kwamba kila mwamini ajifunze mambo yafuatayo:

- Ukweli kuhusu Yesu ni nani na amefanya nini
- Jinsi ya kukaa ndani ya Yesu Kristo kila siku
- Kanuni za msingi za imani yetu ya Kikristo
- Ahadi zake kwetu kama watoto wake
- Jinsi ya kutenda kwa haki

Tunaweza tu kujifunza mambo haya kwa kusoma Maandiko Matakatifu.

M*wanafunzi* ni yule anayepokea Neno la Mungu akiwa na dhumuni la kutii na kuyatumia yale aliyojifunza.

Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. (Yakobo 1:22)

Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lolote nanyi mtatendewa. Hivyo hutukuzwa Baba yangu, kwa vile mzaavyo sana, nanyi mtakuwa wanafunzi wangu. (Yohana 15: 7-8)

Je, ni Wakristo wangapi leo wanaichukulia Neno la Mungu kama orodha ya maoni ambayo wanaweza kuchagua na kuchukua? Ni wangapi wanaelewa kuwa kusudi lao ni kumletea Mungu utukufu? Waamini wangapi hutumia neema ya Mungu bure kutokana na kutotii? Je, tunahuzunika juu ya dhambi zetu, tukitilia mkazo toba na utii, au tunajihesabia haki wenyewe kutokana na ujinga wetu na "makosa" ya dhambi?

Kwa Marekani leo, takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 40 ya Wakristo wako kwenye dozi ya dawa za kupunguza msongo wa mawazo. Katika miaka ishirini na zaidi ya kushauri, nimegundua kuwa watu wengi wanaopata msongo wa mawazo ni ama hawajui, au hawajali yale ambayo Mungu ameyaeleza katika Neno Lake. Kuna matokeo mabaya ya kuishi katika kutokutii. Sisemi kwamba watu wote wanatumia dawa za kupunguza msongo wa mawazo hawatii mapenzi ya Mungu, lakini mitazamo sugu ya kutoridhika, hasira, uchungu, hofu na kadhalika, ni lazima itasababisha msongo wa mawazo.

Wakati mwingine maisha yanaweza kuleta shinikizo kubwa la mawazo, lakini msifu Mungu maana yeye analo jibu. Wagalatia 5:22 inatuambia kwamba kukaa ndani ya Roho Mtakatifu kutasababisha maisha ya upendo, furaha na amani. Haya hayawezi kutokea yote kwa pamoja lakini yatazidi kuonekana kadiri mtu anavyotafuta kutii mapenzi ya Mungu. Je, ni nini hutokea wakati Mkristo, kwa ujinga au uasi, haendi katika mapenzi ya Mungu? Mambo huwa ni kinyume tu, kwani upendo, shangwe, na amani ni mbadala na kuchanganyikiwa, shaka, wasiwasi, na hatimaye msongo wa mawazo. Mungu huruhusu tuteseka kutokana na dhambi na wakati mwingine kutufundisha kwa kutupitisha katika matukio mabaya kwa kuwa yeye ni Mungu mwema, baba mwenye upendo na ambaye hutimiza kazi alioianzisha miongoni mwenu.

Wakati mwingine mateso na shida katika maisha ni kitu cha kawaida tu na chenye kutarajiwa na pengine ni kitu kizuri katika kututuoa kutoka kwenye dhambi, ujinga, au uhuru wetu wa kujitenga na Mungu.

Mungu anaruhusu kuteseka kwa ajili ya dhambi na hata kutufundisha kutokana na matukio kadhaa kwa kuwa yeye ni baba mzuri, mwenye upendo ambaye ni mwaminifu katika ahadi zake ili aweze kumaliza kazi aliyoanza kwa kila mmoja wetu.

> Tena mmeyasahau yale maonyo yasemayo nanyi kama kusema na mwana, Mwanangu, usidharau marudi ya Bwana, wala usizimie moyo ukikemewa naye. Maana yeye ambaye Bwana ampenda humrudi, naye humpiga kila mwana amkubaliye. (Waebrania 12: 5-6)
> Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeianza kazi njema mioyoni mwenu, ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu. (Wafilipi 1: 6)

Mwanafunzi huchukulia Biblia kama maagizo ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu na yanayofaa kutiiwa. Utambuzi wowote wa kutotii ni suala la kufanyiwa toba na huhitaji kuwepo kwa imani thabiti, sala na kutegemea nguvu ya Roho Mtakatifu ili kuanza kuenenda katika haki.

4. ***Mwanafunzi hudhihirika kwa tabia na mwenendo wake, kuelekea mabadiliko ya haraka na ya kudumu ili kufanana na Yesu.***

> Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amehitimu kulingana na mwalimu wake. (Luka 6:40)

Hatutaweza mungu kamwe, kama dini zingine zimefundisha watu kimakosa na hatutaweza kuwa wakamilifu kama Kristo. Yeye ndiye kinga yetu dhidi dhambi, na kwa Roho wake Mtakatifu aliye ndani yetu, maneno na matendo yetu yanapaswa kumtukuza Mungu zaidi na zaidi kila wakati. Mafunzo yanajumuisha kujifunza, msimamo, na mazoezi katika kutenda haki.

Sasa tunajua mwanafunzi ni nani na atakuwa na sifa gani, lakini ni nini kingine kinachohusiana na ufuasi wa kweli? Na tuliangalie hii sasa.

**Mwalimu ni Nani?**

Bwana hutoa karama tofauti kwa wafuasi wake, wengine wameitwa kuwa wachungaji, wahudumu wa vijana, wakurugenzi wa muziki, na kadhalika; *lakini kila muumini anaitwa kuwa mwalimu.* Hii inamaanisha kwamba kila Mkristo anahitaji kufika mahali ambapo anakomaa vya kutosha kuweza kutumia Neno la Mungu kwa mahitaji ya waamini wengine; katika uhusiano wa karibu na kulifanya hili mara kwa mara na kwa lengo mahusui kama Yesu alivyofanya. Kufundisha wanafunzi ni kutumia muda na mwingine, au wengine, kwa kipindi fulani maishani, kuwasaidia kuelewa na kutii Neno la Mungu kwa kuwatia moyo, kuwasihi, na muhimu zaidi, *kuwa mfano kwao*. Kumbuka, Mathayo 28:19, inasema *"fanyeni wanafunzi kwa Mataifa yote."* Katika andiko hili, yote inamaanisha yote, na hiyo ndiyo maana halisi ya yote!

Je! Wachungaji, viongozi wa ibada, viongozi wa masomo ya Biblia, au wahudumu wengine wa kawaida wameondolewa kwenye wito huu? Hapana; kwa hakika, Mungu anatarajia mengi kutoka kwa wale wanaoongoza. Angalia Maandiko yanasemavyo kuhusu hii:

> Amin, amin, nawaambieni ninyi, mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala mtumwa si mkuu kuliko yeye aliyempeleka." (Yohana 13:16)

> Katika mambo yote unajionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema; na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na usahivu. " (Tito 2: 7)
> Wakumbukeni wale waliokuwa wakiwaongoza, waliowaambia Neno la Mungu; tena kwa kuuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iigeni Imani yao. (Waebrania 13: 7)

Yesu alikuwa mwalimu bora zaidi, lakini wanafunzi mara nyingi walimwuliza, "Ulimaanisha nini?" Utayari wake wa kukatisha mafundisho na kuwaelezea zaidi na kujibu maswali yao, ilionyesha kuwa mambo mengine katika huduma, kama vile uponyaji au kuhubiri, hayakuwa muhimu kuliko kuwafundisha! Maisha ya Yesu yalifunua thamani na kipaumbele ambacho Mungu huweka juu ya kuwafundisha wengine.

Katika Mathayo 9: 35-38, Yesu aliwaambia mitume waombee watendakazi wengi zaidi:

> Naye Yesu alikuwa akazunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao na kuihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na madhaifu ya kila aina. Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji. Ndipo alipowaambia wanafunzi wake; mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno apelike watendakazi katika mavuno yake.

Mfanyakazi ni mtendakazi wa kiroho ambaye ni mwanafunzi na mwalimu pia. Kila muumini anastahili katika dhana hii ya mfanyakazi. Lakini ni waamini wangapi wanaomfuata Kristo kwa uaminifu kiasi kwamba wanastahili kuongoza, kufundisha, au kuwa mfano kwa mtu mchanga katika imani? Kila Mkristo ni mfanyakazi anayeweza kutendakazi hii. Yesu alikuwa aliwatafuta watu hao wakati ule, na sasa anawatafuta pia. Ni Yesu Kristo ndiye ambaye huokoa mtu, kisha hapo ndipo sehemu yetu inapoanzia, kuwafundisha hadi wakomae kiimani kama alivyofanya yeye. Ni kweli tunahitaji kutangaza Injili na kutoa mialiko ya kumpokea Yesu Kristo, lakini muhimu pia ni kufanya watu kuwa wanafunzi! Je! Tunafanyaje hii?

"Kufanya watu kuwa mwanafunzi" ni kuwasaidia wengine kuiga mfano wa Kristo. Hili huanzia kwa uongozi,

> Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu, kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe. (Waefeso 4: 11-12)

Wazo hapa ni kwamba, viongozi wa kanisa wanapoishi maisha ya Kikristo kwa kufuata vyema mafundisho ya Yesu, wanaweza kufundisha na kuhimiza wengine pia ili nao waweze, kufundisha na kuhimiza; wakirisisha ujuzi na nguvu ambayo Mungu ameionyesha katika maisha yao. Hii basi, huleta imani na ukomavu kwa wengine ili waweze kugusa maisha ya wengine kwa zamu (2 Timotheo 2: 2). Unapojifunza ufafanuzi wa dhana ifuatayo, angalia sana vidokezo vilivyopigiwa mstari vinavyohusiana na kufanya watu kuwa wanafunzi. Ukiangalia kwa karibu, utagundua kuwa ufafanuzi huu unaelezea kusudi na mchakato ambao Kristo aliuwasilisha kwa wanafunzi Wake. Chukua muda kutafakari juu ya ufafanuzi huu.

> *Fanya Wanafunzi*: (kitenzi cha Kigiriki) "Matheteuo," maana yake ni kufanya mwanafunzi (Mathayo 28:19; Matendo 14:21); kuelekeza kwa kusudi la kufanya mwanafunzi (Mathayo 13:52). Siyo sawa kabisa na kusema "kufanya waongofu," ingawa kwa hakia inaweza kutumika. Neno "fanya wanafunzi" linaweka mkazo zaidi juu ya ukweli kwamba akili, moyo na mapenzi, lazima viwe kwa ajili Mungu [1] kwa kuwaelekeza waamini wapya juu ya jinsi ya kumfuata Yesu, kujitiisha katika enzi ya Yesu, na kuchukua utume wake wa huduma ya huruma. [2] Inajumuisha pia kuwaleta watu katika uhusiano na Yesu kama wanafunzi, kuwafundisha na kuwafanya wachukue nira yake ya mafundisho kuwa kama mamlaka kwao, kukubali maneno yake kuwa ndiyo kweli, na kujitiisha kwa mapenzi yake kuwa ndicho kitu sahihi. (Mathayo 11:29) [3]

Paulo amekuwa mfano halisi wa tabia hii katika huduma yake yote. Alitumia miaka mitatu huko Efeso akiwafundisha waamini katika "shauri lote la Mungu," ili waweze kukomaa katika Kristo (Matendo 20: 27-31). Pia aliwafundisha viongozi na kuwaelekeza kufanya vivyo hivyo, kutumia nguvu zao na wakati wao kuwafundisha waamini wengine (2 Timotheo 2: 2). Paulo na Barnaba walirudi kwa waamini huko Lustra, Ikoniamu, na Antiokia kwa kusudi la "kuwaimarisha wanafunzi kiroho na kuwahimiza waendelee katika Imani yao" (Matendo. 14: 21–22). Kuimarisha kunamaanisha walishirikishana Neno la Mungu wakati kuhimiza inamaanisha waliwasihi na kuwatia moyo waamini kutii na kuvumilia amri za Kristo.

Sasa tunafika kwenye sehemu ya tatu ya Mpango wa Uanafunzi wa FDM -kufuata mfano wa Kristo kupitia unganisho la makusudi.

## KUIGA MFANO WA YESU

Sehemu ya tatu ya kuwafanya watu kuwa wanafunzi ni kuiga mfano wa Kristo kwa njia ya uhusiano wa kudhamiria. Yesu anatuonyesha mfano halisi wa jinsi inavyokuwa katika kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.

> Kwa maana nimewapa mfano huu, ili mtende kama vile nilivyowatendea ninyi. Amin, amin, nawaambia, mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala yule aliyetumwa si mkuu kuliko yeye aliyempeleka. Ikiwa wajua mambo haya, umebarikiwa ukiyafanya. (Yohana 13:15-17)

Alichagua wanaume kumi na wawili na kuwafundisha yeye mwenyewe; walikuwa waanzilishi wa Kanisa lake baada ya Roho Mtakatifu kuja kukaa ndani yao, kulingana na ahadi ya Yesu. Wanaume hawa walijimimina kwa wengine kama viongozi waaminifu na waalimu wa yote ambayo Yesu alikuwa amewafundisha.

Kufanya watu kuwa wanafunzi, au unafunzi, ni mchakato tunaofuata kuwasaidia watu kuiga mfano wa Kristo. Ingawa maneno haya mahsusi hayatumiwi katika Biblia, wazo hilo linawasilishwa wazi na njia ambayo Yesu aliitumia kuwafundisha wafuasi wake na inajidhihirisha pia katika Maandiko yote, kama Mathayo 28: 19-20 na mistari mingine ya Agano Jipya. Utafiti zaidi utaonyesha uhusiano kati ya ufafanuzi tuliyousoma na mchakato wa kuwafanya watu kuwa wanafunzi, zaidi sana kama unawahusisha wale walio katika mazingira yako. Ufafanuzi wa kufanya watu kuwa wanafunzi kutoka kwa Greg Ogden unaelezea pia dhana ya Ki-Biblia tunayopaswa kuwa tunaitumia kama viongozi wa makanisa na waamini.

> *Kufanya watu kuwa wanafunzi/Uanafunzi*: "Ni <u>uhusiano wa kudhamiria</u> ambao unatufanya <u>kuwa pamoja</u> na wanafunzi wengine <u>kuhimizana, kuwezeshana na kukosoana kwa upendo ili tuweze kukua na kukomaa katika Kristo</u>. Hii hujumuisha kumuwezesha mwanafunzi kufundisha wengine pia."

Ingawa ufafanuzi huu unahusiana na uanafunzi wa aina zote, ningependa kuuhusisha sana na viongozi katika Kanisa na uhusiano wao na makusanyiko. Picha hii ya uanafunzi inaelezea kile ambacho Kanisa linapaswa kuwa linakifanya, na inafafanua kile ambacho Kristo alikifanya na wanafunzi wake. Kuwafundisha kweli waamini katika Kanisa kunamaanisha kuwa na uhusiano mahsusi na wao; hili ni jukumu letu sote. Yesu aliwaita wanafunzi wake wamfuate, au watembee sambamba naye, lakini alikuwa na kusudi maalum kwa yeye kuwa mbele yao. Lazima tutambue kuwa uhusiano wa kukusudia haufanyiki kwa bahati mbaya; kuna haja ya kuwa na mpango wa mapema ambao unadumishwa daima. Hiki ndicho kinachozungumziwa katika kijitabu hiki; yaani, kukupa mpango ambao utakusaidia kuanza mchakato wa uanafunzi.

Mwanafunzi hawezi kukua katika imani yake bila kuwekeza muda na nia katika kujifunza. Familia ziko matatani leo kwa sababu ama hawajui taarifa kamili zinazoweza kuwasaidia, au hawaenendi kwa kujifunza na kufuata Neno la Mungu. Wanandoa wengi wa Kikristo wanaanzisha uhusiano wa viwango vya chini sana kulinganisha na shauku ya Mungu anayoitaka kwao. Ni wangapi hawajui wapi wapate msaada wanaohitaji? Inavyoonekana, mapumziko ya mwisho wa juma, vitabu, na hata ushauri sio utatuzi wa matatizo yao.

Je! Yesu alionyesha jibu bora litakuwa kwenye vitabu na mapumziko? Hapana, yeye anasema,

> Kwa kuwa nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyowatendea nanyi mtende hivyo. (Yohana 13:15)

Kanisa linahitaji kuelewa kuwa mapumziko na ushauri na saha ni msaada, lakini siyo mbadala wa uanafunzi linapokuja suala la kuwaletea watu mafanikio katika maisha ya Kikristo.

Yesu daima anasimamia kuwa kwa mfano wake na uhusiano wa kibinafsi na yeye kama siraha ya kwanza ya vita dhidi ya dhambi. Hii inahitaji muda wa kutosha katika uhusiano na mtu ambaye yuko tayari kuwekeza katika ukuaji wa kiroho na maendeleo ya watu wengine. Huu ni uanafunzi yaani, juhudi ya muumini ambaye amejaribiwa kupitia mateso na majaribu na amejifunza utii, ni mtu ambaye sasa anauwezo na yuko tayari kuwa pamoja na mwingine, au wengine, kuwaongoza, kuwafundisha na kuwaimarisha.

Inabidi uangalie tu maisha ya Yesu kujua jinsi alivyowafundisha wengine. Aliwahudumia kila wakati wale walio karibu naye; Mitume wake pia ambao waliendelea kumimina maisha yao kwa wengine, wakifundisha na kuonyesha mapenzi ya Mungu. Orodha ya mifano ni udhihirisho wa wazi; uanafunzi ni mfano ambao Yesu aliweka uendelezwe na wafuasi wake waaminifu.

Tunaposoma Injili, tunaona jinsi Kristo alivyomimina maisha yake kwa wanaume kumi na wawili maalum ambao aliwateua na wakakubali kufuatana naye. Aliwafundisha kwa lengo mahsusi kabisa kwa kipindi cha miaka mitatu. Walijifunza, walitazama, waliuliza maswali, walisikiliza mafundisho yake na hata wakaanza kuiga tabia zake. Popote alipokwenda, hilo ndilo lilikuwa darasa lao. Yesu aliwafundisha kujua somo moja la maisha hadi jingine; kila walipokuwa hawaelewi kitu, alisimama na kuelezea zaidi (Marko 4:34). Alifafanua zaidi wakati ambao wanakuwa hawakuelewa kitu (Marko 8: 15-21); na alikemea ukosefu wao wa imani wakati amabo waliihitaji (Marko 9: 19–29).

Mara Yesu alipoendelea katika huduma yake katika makusanyiko, aliwaalika wote waliokuja kwake kumfuata, akiwaasa, "Fuateni mfano wangu, jifunzeni kutoka kwangu, muwe mwanafunzi wangu." Vivyo hivyo, waamini wote wanaalikwa kufuata mfano wa Kristo, ambayo inamaanisha kudhamiria kuwafikia kwa moyo thabiti ili kuwafundisha, kuwafanya kuwa wanafunzi na kuwaimarisha katika imani.

Katika sehemu inayofuata, tunaangalia makundi mawili maalum ya watu ambao wanahitaji dhamira yetu, makundi hayo ni: uongozi katika Kanisa, ambao ni pamoja na wachungaji, mashemasi, wafanyikazi na viongozi wa kawaida; na kundi la pili ni kila muumini, ambao ndilo kundi letu. Je, ni kwa namna gani tunaweza kufikia uhitaji huu wa uanafunzi kwao? Hebu tuangalie.

## FANYA KILA KIONGOZI AWE MWANAFUNZI

Je! Huduma yenye ufanisi hutokea tu? Hapana! Lazima kuwe na maono (Mithali 29:18) na mpango maalum ulioandaliwa. Mungu anatuonya dhidi ya kuchanganyikiwa (1Wakorintho 14:33); wale walio katika uongozi wanajua kuwa nia njema zinaweza kuharibiwa na shughuli nyingi, mipango na juhudi zingine ambazo zinatuondoa katika kusudi kuu. Ikiwa tunapaswa kutimiza wito wa Mungu wa uanafunzi ndani ya Makanisa yetu, lazima kuwe na maono, mipango ya kimkakati na mikakati inayotekelezeka.

Kiongozi katika Kanisa anapaswa kujua Neno la Mungu na kujitolea kuishi katika utii na nguvu. Hakuna mtu aliye mkamilifu, lakini mwamini lazima ayalewe maisha ya uanafunzi na aenende katika njia hiyo ili kuweza kumuongoza mwingine. Kama matini zetu za kufundishia zinavyoonyesha, kuna mchakato na utaratibu wa huduma ya uanafunzi. Kuna Wakristo wengi, hata viongozi katika Kanisa, ambao hawajajifunza wenyewe juu ya umuhimu wa ibada za kila siku, kukaa ndani ya Kristo, ukweli wa msingi wa imani na maagizo ya Ki-Biblia juu ya kuwahudumia wenzi na watoto. Hivyo, tunapendekeza kwamba viongozi wapitie mafunzo haya kwanza.

Kwa nini hili liwe la kwanza? Kwa sababu waamini hawawezi kuongoza watu wengine katika mtindo wa maisha ambao hata wao hawauelewi na hawauishi. Viongozi wanapaswa kujua na kufuata mapenzi ya Mungu na njia zake katika maisha yao wenyewe; vinginevyo, kutakuwa na athari mbaya zinazoonekana kwa sababu misingi yao siyo imara (Tito 2: 7; 1 Timotheo 3: 4-12).

Wachungaji wanahimizwa kusoma vitabu vya kujifunzia tunavyotoa na kujionea wenyewe faida za somo hili. Kisha, kwa matumaini na imani, unaweza kuanza kuifundisha timu yako ya uongozi. Sisi katika FDM tunapendekeza usome vitabu vyetu vitatu vya kujifunzia:

*Christian Foundational Truths: A Strong Foundation for a Disciple, Marriage Is a Ministry series na Parenting Is a Ministry series.*

Nakala za maunzi laini (kielektroniki) ni bure kwenye www.discipleshipworkbooks.com, au nakala za machapisho zinapatikana katika www.FDM.world.

Mzee au kiongozi ambaye amesoma kitabu hiki, anazitumia kanuni hizo kwa uaminifu, na yuko tayari kuendelea kujifunza anaweza kuanza kuwafundisha wengine. Kwa miaka kumi iliyopita, tumeshuhudia mzunguko huu ukiendelea katika Makanisa ndani ya nchi, kitaifa na kimataifa. Huleta tumaini, mabadiliko na kutukuwa kwa nguvu kuu ya Mungu kwa waamini wanaohusishwa.

Wakati tunaendelea kuwafundisha wengine kwa kutumia matini hizi, ufuatiliaji ni muhimu kuhakikisha kuwa wanatumia kanuni hizo katika maisha na kwenye familia zao. Tumegundua kuwa uthabiti ni ngumu bila uwajibikaji; Wakristo wengi, hata wale walio katika uongozi wa Kanisa, hawaelewi matokeo ya kuvunja maagizo ya Mungu katika maeneo haya. Mchungaji

anahitaji kuwa na bidii na kueleweshwa wazi kwamba ukweli katika Neno la Mungu ni lazima na sio kitu kinachopendekezwa tu.

> BWANA, Mkombozi wako, Mtakatifu wa Israeli, asema hivi: Mimi ni BWANA, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida, nikuongozaye kwa njia ukupasayo kuifuata. Laiti ungalisikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji, na haki yako kama mawimbi ya bahari. Tena wazao wako wangelikuwa kama mchanga, na hao walitoka katika tumbo lako kama chembe zake. Jina lake lisingekatwa wala kufutwa mbele zangu. " (Isaya 48: 17-19)

Mungu anahitaji sana kutukuzwa ndani yetu kupitia kila mtoto wake. Sio shughuli nyingi ambayo hutufanya sisi kuwa wahudumu bora wa Kristo, bali ni kutenda yaliyo mapenzi ya Mungu (1 Samweli 15: 22-23). Mungu hutoa hata maelekezo kwa wachungaji kuhusu tabia ya wale ambao wanaweza kufikiriwa kuwa viongozi.

> Yaani mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu? (1 Timotheo 3: 5)
>
> Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya mashemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. (1 Timotheo 3:10)

"Jaribiwa kwanza," maana yake ni kupitia msimu wa kutii kwa uaminifu katika kutenda mapenzi ya Mungu katika maeneo haya maalum. Mchungaji ana mamlaka na amewajibishwa na Mungu kufundisha uongozi wake. Kondoo ambao Bwana amewapa vipawa vya kipekee kwa kuujenga mwili lazima kwanza wafanywe wanafunzi na wapewe msimu kuonyesha nia yao ya kuwa watiifu. Ni muhimu sana kwamba mchungaji anapaswa kuwasihi viongozi wao kuyaona maagizo haya kama vipaumbele muhimu ambavyo vinapaswa kutekelezwa katika maisha yao.

> Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo, imani na usafi. (1 Timotheo 4:12)

> Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshiriki wa utukufu utakaofunuliwa baadaye; lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu na kulisimamia, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Na Mchungaji Mkuu atakapodhihiriswa, mtaipokea taji ya utukufu ile isiyokauka. (1 Petro 5: 1-4)

> Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu, kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi; akaaye ndani yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote. Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na hunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea. Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. Hivyo hutukuzwa Baba yangu kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu. (Yohana 15: 4–8)

Ni kawaida kwa wachungaji kukutana na upinzani wakati wanapowasilisha kitini hiki kwa uongozi wao. Wengine wanaweza kuhisi kuchoshwa, wengine kutishiwa na wengine wanaweza kuchukulia kama siyo lazima au kufikiria kuwa hawaitaji msaada. Wahakikishie wenye mashaka kwamba unafuata maagizo ya Mungu katika yaliyoko katika 1 Timotheo 3: 1-12 na Tito 2: 7. Kama viongozi, wana wajibu kwa Mungu kwa kila namna ya kutoa ushauri, kufundisha, au kumshauri mtu. Inachusha haswa kwa mchungaji kuwajibishwa kutokana na maneno na matendo yao, kwani wanahudumu kwa uwezo wake.

Wakati watu wapya wanapotaka kushiri katika uongozi wa Kanisa, mchungaji au mtu mwingine aliyeteuliwa anapaswa kuwafundisha kupitia kitini hiki na kuruhusu msimu wa matazamio. Wanapaswa kutumia kanuni hizi kwa uaminifu na kuonyesha uelewa wa ukweli ambao wamejifunza kabla ya kupewa nafasi. Tunatamani kila wakati waelekezwe kwa kutumia vitabu vyote vitatu vya kujifuanzia hata kama hawajaoa/kuolewa au hawana watoto. Hii inawaandaa kuhudumia au kufundisha katika maeneo ambayo kundi linaweza kuwa linajitahidi huduma hiyo.

Wachungaji wengi hawajafundishwa na hawajapata athari ya muumini aliyekomaa akijimimina kwao katika msimu wa matazamio kwa kuonyesha mfano ambao Yesu na wanafunzi wake walianzisha. Siyo tu kumpa mtu kitabu halafu unakutana nao muda wowote kuuliza kile ambacho wamejifunza. Wala siyo kuwaweka darasani au kuwataka kupitia mfuatano wa video peke yao. Kufundisha kunahusisha kusoma mara kwa mara na kutafakari kwa pamoja ukweli wa Biblia, kusaidia kutambua maeneo yenye shida na kuweka malengo, pamoja na kuweka msingi wa uwajibikaji. Vitabu vyetu vya kufundishia vimeandaliwa kutimiza aina hii ya ushirika, kufundisha, na kufanya ufuatiliaji.

Kwa kutambulisha matini hizi na kuzitumia kwa uaminifu, mchungaji anafuata mfano wa Yesu wa kufundisha na kuelimisha wanafunzi. Tunajua kwa uzoefu kwamba wachungaji wanaofanya hivi wanaona ukuaji mzuri wa kiroho katika kundi. Tunaelewa kuwa wengi wanaweza kuhisi mchakato huu unachukua muda wetu mwingi, kuliko maisha yetu yenye shughuli nyingi yanavyoweza kuruhusu, lakini msisitizo wetu ni kwamba mtindo huu wa maisha na ukweli wa Ki-Bibiblia unaotokana na mazoezi haya hubadilisha maisha! Ikiwa Bwana wetu na mitume walitumia njia hii ya kufundisha kusaidia waamini kujua na kufuata njia na mapenzi ya Mungu, basi tunawezaje kuhalalisha kutotenga wakati? Kumbuka, kufundisha ni kwa kila muumini na imeamriwa na Mungu. Viongozi wanapaswa kuongoza kwa mfano.

> Kwa maana nimewapa mfano kwamba mnapaswa kufanya kama vile nilivyowatendea ninyi. Amin, amin, nawaambia, Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake; wala yule aliyetumwa si mkuu kuliko yule aliyemtuma. Ikiwa unajua mambo haya, umebarikiwa ukiyafanya. (Yohana 13: 15-17)

## FANYA KILA MUUMINI AWE MWANAFUNZI

Agizo Kuu la Yesu, "Basi nendeni mkafanye wanafunzi" (Mathayo 28:19-20), inawahusu waamini wote. Lakini Wakristo wengi hawaelekei kuwa wengi huchukulia kama kikundi cha wasomi, ambacho hakiwastahili. Wengi wanaamini kuwa darasa la uanafunzi ni mahali ambapo wangejifunza misingi ya imani ya Kikristo. Makanisa mengi huchukulia kufanya watu kuwa wanafunzi darasa la muda mfupi, lakini hiki siyo ambacho Yesu alimaanisha aliposema: "fanyeni wanafunzi." Yeye ni mfano wetu, na njia yake ilikuwa mahsusi sana na ilikuwa endelevu. Kristo alikusudia wafuasi wake washirikiane kwa kufundishana, kutiana moyo na kuwajibishana. Biblia inazungumzia juu ya kuomba pamoja na hata kuungama dhambi zetu kwa kila mmoja. Waamini wangapi wanaishi mtindo huu wa maisha, au hata wanajua kuwa huu ni mpango wa Mungu kwao? Kila Mkristo anahitaji kujua kwamba Kristo amewaita kuwa mwanafunzi. Na kila Mkristo anahitaji kujua kwamba wao pia wameitwa "kufanya watu kuwa wanafunzi." Kanisa linapaswa kuwa nguvu kubwa katika uinjilishaji huu na kuwaandaa watoto wa Mungu.

Katika Kitabu cha Tito 2: 1–10, Paulo anampa Tito pendekezo la kufundisha ndani ya Kanisa; waamini wazee walipaswa kufundisha na kuwasihi vijana, huku wakihakikisha kwamba tabia zao daima ni mfano wa utakatifu na matendo mema kulingana na mafundisho imara na kujizuia. Na katika Kitabu cha Waebrania 5: 12–14, mwandishi anaonyesha kwamba waamini wanapaswa kukomaa, siyo kuwa ni watoto wachanga, lakini waweze kula nyama ya Neno la Mungu. Aina hii ya ukuaji wa kiroho ni alama ya ufuasi. Wito ni kushiriki katika maisha ya wengine na kupata wakati na kuwasaidia kujifunza jinsi ya kutenda mapenzi ya Mungu maishani mwao. Tunaona pia kwamba wito huu hauzuiliwi kwa mchungaji na wafanyikazi wake.

Deni kubwa la mchungaji na wafanyikazi wake kwenye kundi ni jukumu la kuufanya mpango huu wa uanafunzi uendelee. Kila mwamini anapaswa kufurahiya matarajio ya kuwa mwanafunzi aliyejitolea wa Bwana wao Yesu Kristo. Uongozi unahitaji kuiga mfano huu, lakini bila maono na mikakati iliyowekwa dhahiri na mchungaji, hili haliwezi kutokea. Vitabu vya kufundishia tunavyotoa vimejazwa na maneno na ukweli wa Mungu, ni nyenzo za kutumia kwa ukuaji wa kiroho, kwa kuwawezesha watakatifu kuzingatia vipaumbele vitatu ambavyo Mungu ameweka katika maisha yao. Mungu huzungumza juu ya hitaji na thamani ya kuishi kwa nidhamu kupitia Neno Lake. Ukifuata maagizo na hatua zilizowekwa kwenye matini hizi, mifumo itakuwa mipya na maisha yatabadilika. Ufuatiliaji ni sehemu muhimu ya mchakato huu au mbinu na imejikita katika Maandiko Matakatifu. Ufuatiliaji hudhibitisha kuwa uanafunzi ni mchakato endelevu

Makanisa mengi yana mipango au huduma maalum zinazolenga kila hatua ya maisha ya washirika wao. Hii ni nzuri, lakini hiki ndicho kitu pekee kinachofundishwa kwao ambacho ni muhimu sana. Acha tuangalie huduma nyingine za muhimu na jinsi unavyoweza kutumia matini za FDM kwa mchakato wako wa uanafunzi katika maeneo haya. Lengo ni kulifikia kundi lako mahali lilipo.

**Madarasa ya Ndoa na Malezi**

Namna nzuri ya kuanza uanafunzi katika eneo hili ni kwa kutoa madarasa ya kila robo mwaka ambayo hupitia kila kitabu, kama kinavyotumika. Kwa mzunguko huu, wenzi ambao wanaweza kuhitaji msaada, huweza kuingia katika darasa jipya mara moja kabla ya tatizo lao halijawa kubwa zaidi. Kiongozi anapaswa kuwa mtu ambaye tayari ana uelewa wa yaliyomo katika kitini hiki na kuziishi kanuni hizi katika maisha yao. Mahali pa kujifunzia ni ya hiari yako, iwe kanisani au mazingira ya nyumbani. Madarasa haya ni mazuri kwa kila rika na hatua za ndoa, na pia kwa wenzi wa kabla ya ndoa.

Kadiri wanandoa wanapohusika katika madarasa, viongozi wanahitaji kuwa katika sala kwamba Mungu awainue wahitimu kuwa washauri wa ndoa ambao wanaweza kuungana pamoja na kuwafundisha wenzi wengine. Inatarajiwa kuwa mambo yanaweza kujitokeza vinginevyo ambapo msaada zaidi unaweza kuhitajika, kama vile ushauri na saha na ufundishaji wa mtu mmoja mmoja. Hadi sasa, tunaomba Mungu kwamba uwe unatambua maono ambayo yanaweza kuwa njia yenye kuzaa matunda na maarifa mengi ya kuhudumia kundi lako. Waamini wanaposhiriki zaidi, watagundua karama ambazo Roho Mtakatifu amewapa kwa ajili ya kuimarisha shirika zao. Watu wanapoelewa mapenzi ya Mungu kwao kama watoto wake, huduma itaongezeka na utashuhudia furaha na maisha ya ushindi kati ya wale wanaoitikia wito wa kuwa wanafunzi wake.

Kama sehemu ya mchakato wa ufuatiliaji, jihadharini na tatizo lilizoeleka la watu fulani kuwa na majukumu makubwa kuliko kawaida. Angalia kuenea kwa Roho wa Mungu kwa watu wapya ambao hawawezi kuwa na vikwazo katika kuwafundisha wengine. Mara tu unapoanza na huduma hii ya ndoa na malezi, ni wazi kuwa mambo mengi ya zamani yanayoumiza kwa wanandoa wanaweza kukosa mapokeo mazuri, wakipinga mabadiliko; lengo ni kuzuia yasiendelee, siyo kuingilia kati baada ya watu kuwa katika mfumo kamili wa maisha usiofaa. Kutumia kitini hiki kutakusadikisha kujua kwamba hitaji la uanafunzi wa ndoa ni kubwa badala ya kila mara kuweka wazi mifumo na mitazamo hasi ya muda mrefu katika vyumba vya ushauri na saha.

**Ushauri na Saha**

Ushauri na saha ni fursa nzuri zaidi ya kuwasilisha matini na vitabu vyetu vya mafunzo ya Ki Biblia. Kwa mfano, wanandoa huja ndani, na ni Dhahiri kabisa mke anawezakuwa anajisikia kuchukizwa sana, au mume kuwa anapenda kazi kupita kiasi. Watu wanapokuja kwa mshauri, ni matumaini kuwa wako tayari kufanya kazi binafsi ili waweze kutatua matatizo yao. Michakato ya uanafunzi inayolenga ushauri na saha pia itafunua mzizi wa kiroho unaohusiana na tatizo hilo; inafichua ujinga na tabia za dhambi walizoanzisha. Kuondoa dalili za tatizo au kupoteza muda kusikiliza uovu wa mwili usio na maana havimsaidii mtu yeyote. Mzizi wa matatizo mengi ya ndoa ni matokeo ya kutokujua mapenzi ya Mungu na njia za kuwa na ndoa bora pamoja na ubinafsi.

Jukumu la mshauri anayefundisha hujumuisha:

- Waelekeze kwa Yesu na Neno lake kwa wokovu, uponyaji na mafundisho.
- Saidia mtu aelewa kwa nini na jinsi gani ambavyo tatizo limeingia katika maisha yake.
- Wafundishe kuenenda katika haki na kuzingatia vitu ambavyo Mungu amewapa, yote kulingana na Neno lake.
- Tafuta msamaha na upatanisho pale vinapohitajika.
- Elekeza upendo, kutiana moyo, kuchukuliana na kuanza upya.

Vitabu vyetu vya kujifunzia vina faida kwa mshauri na mshauriwa. Vimeandaliwa kwa namna ya kuweza kufundisha ukweli wa Mungu kwa mtu kujifunza yeye mwenyewe au kwa kupewa kazi za kuwasaidia kuelewa na kutumia kile wanachojifunza. Watu ambao kweli wanataka kubadilika watatenga muda wa kufanya kazi hiyo kila wiki. Kumbuka, Mungu hawezi kufanya kwa muujiza kile ambacho kinatupasa kutenda kwa utii wetu. Ikiwa hawakuwa tayari kufanya kazi yao ya nyumbani, utawafanyia nini? Ni Neno la Mungu pamoja na hamu yao ya kufuata mapenzi yake ndiyo ambayo huleta mabadiliko.

Mtu ambaye hayuko tayari kufanya kazi ya nyumbani lakini anataka kutumia wakati wako kwa kulalamika, kuhukumu wengine, au kutoa visingizio juu ya kwanini hawezi kufanya kile ambacho Mungu anamwaambia kwa wazi, anamdhihaki Mungu kwa kificho. Mungu si mwongo; Neno lake, Roho Mtakatifu na nia ya kutii; vyote ni vitu anavyohitaji mtu ili awekwe huru na kuweka maisha yake sawa. Unahitaji kusimama juu ya ukweli huo.

> Pasipo na maono, watu huacha kijizuia; bali ana heri mtu yule aishikae sheria. (Mithali 29:18)

Omba na utafute mwongozo wa Bwana katika kuwakuza wanafunzi ili kusaidia kushauri na kuwafundisha wengine. Washauri lazima wawe na nyenzo za kufundishia na vitabu vya kujifunzia vinavyofaa ambavyo hujumuisha eneo pana la maarifa kuliko, mathalani, chuki, hasira, au ujuzi wa mawasiliano. Mara nyingi, kuwa na tatizo fulani ni dalili za kuwa mjinga katika eneo jingine la maisha, linalohusisha; ndoa, malezi, au kutosamehe. Kushughulikia suala moja (inaweza) isielekeze katika mzizi wa msingi wa maisha ya kiroho yasiyofaa. Kumbuka, matatizo mengi yanatokana na ujinga, uasi, au masuala ya kiroho. Mungu ana jibu kwa mtu yeyote ambaye atajifunza na anatamani kumfuata.

Ushauri mzuri utafanya yafuatayo:

1. Utaleta uelewa wa chanzo cha tatizo: dhambi, ambayo hutokana na kutotii, kutokujua eneo fulani la Neno la Mungu (au kutosamehe).
2. Utasaidia kutambua matokeo yanayotokana na tatizo: mielekeo ya dhambi, tabia, mienendo mibaya, hasira, tabia zisizo za Kimungu, kutunza ubaya, mawasiliano duni, na kadhalika.

Matini nzuri za mafunzo ya Ki-Biblia zinakusaidia wewe katika kuzifafanua kanuni za Mungu na kuuelekeza msingi wa tatizo. Matini hutoa taarifa kuhusu uelewa na mienendo sahihi. Hayo uhusisha ndoa na masuala ya malezi. Matini zetu za bure mtandaoni yatakusaidia katika ushauri wako na saha; unaweza kutembelea tovuti zetu zote mbili ili kujua zaidi: www.fdm.world na www.discipleshipworkbooks.com.

**Huduma za Kifamilia**

Katika kuwaweka watoto wakfu kwa Mungu, unamuomba Mungu ambariki mtoto na familia, lakini hii liwe wazi pia kwa umma wa wazazi wenye nia ya kumtoa mtoto kwa Bwana (Mithali 22: 6). Mantiki hapa ni kulea mtoto kama Bwana anavyofundisha katika Neno lake. Sisi, Kanisa, lazima tuchukulie hili kwa uzito, na ikiwa tutafanya hivyo, basi lazima kuwe na mpango katika maalum ambao unatoa maagizo ya Ki-Biblia juu ya jinsi ya kulea mtoto. Kama utakavyojifunza kutoka katika vitabu vyetu vya kujifunzia, hii inajumisha mambo zaidi ya kuwaleta kwenye shule ya Jumapili, kanisani, au hata kuwa na ibada nyumbani. Malezi ni changamoto, na ikiwa wazazi hawakai ndani ya Yesu kila siku kama wenzi na kutenda mapenzi yake, wanawezaje kufanikiwa?

Kama tulivyosema hapo awali, watu hujifundisha kwa miito yao, wengine kwa miaka mingi, na pia inachukua muda na kupata uzoefu kabla ya mwajiri kumpa mwajiriwa jukumu kubwa. Wazazi wengi hawana mafunzo ya malezi licha ya ukweli kwamba Neno la Mungu limejaa mafundisho. Kabla ya kumtoa mtoto mchanga, viongozi wa kanisa wanapaswa kuandaa darasa la malezi au kikundi cha kuwapitisha katika kitabu cha mafunzo ya malezi. Kufundisha wazazi jinsi ya kujenga mazingira ya upendo nyumbani, kuwafundisha watoto wao wenyewe, kuwa na muda wa maombi na kuwa na utaratibu wa umoja na sahihi kwa ajili ya nidhamu; jambo ambalo ni muhimu sana kwa ukuaji wa mtoto. Takwimu zinaonyesha kuwa wakati watoto wengi wa leo wanaondoka nyumbani, ndiyo wanazidi kujitenga mbali na imani katika Mungu.

Wakati watu wanapopitia baraka za uanafunzi katika maeneo haya, pia huweka msingi wa uelewa na maono ya kuwafundisha wengine. Unapoelezea kuwa mtoto huyu ametolewa na Mungu kwa sababu mtoto ni zawadi iliyowekwa chini ya uangalizi wao, ili kulelewa kulingana na maagizo yake, wataona hitaji la kufundishwa.

Tena, wazazi lazima wawe mfano wa utakatifu binafsi, kinyume chake, matumizi ya kanuni za malezi hayatakuwa mzuri. Ufundishaji siyo utoaji wa mfuatano wa video na vitabu vya kufundishia ili waweze kupitia peke yao; bali inahitaji kwamba mtu awafuatilie baada ya kila somo. Watu wanapokuwa hawajasaidiwa, mara nyingi hupotea katika mambo yao mengine, pia wanaweza kuvurugwa na habari kutoka kwa vyanzo visivyo vya K-ibiblia. Kuna hatua thabiti na ngumu pia zinatakiwa kufuatwa.

**Huduma za Vijana na Kutoa Ushauri**

Mchungaji wa vijana mara nyingi ana ufahamu muhimu juu ya familia za watoto anaowachunga. Ni muhimu kuwa na mawasiliano kati ya mchungaji wa vijana, mchungaji wa familia (ikiwa inafaa), na mchungaji mwandamizi ili kuwatambua wale wanaopata matatizo. Hii inasaidia kwa kuwa ni juhudi za kuzifikia familia zinazopambana na masuala ya malezi. Paulo aliwaambia viongozi wa Efeso,

> Jifunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha Kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe. (Matendo 20:28)

Hii ndio sababu ni muhimu sana kufundisha wachungaji wa vijana na wasaidizi katika uanafunzi binafsi na mpango wa Mungu wa kulea watoto. Wachungaji wa vijana wanahitaji mafunzo haya ili kuhudumia vyema kwa kutambua shida na kutoa suluhisho za Ki- Biblia au kupeleka wazazi kwa watu ambao wanaweza kuwafundisha katika eneo hili.

Ni kawaida kwa wazazi kupiga simu au kukutana na mchungaji wa vijana ili kupata mitazamo wake au hata ushauri juu ya kushughulika na mtoto. Mchungaji wa vijana mara nyingi ana nafasi ya kumsaidia mtoto aendelee kushikamana na Bwana na wazazi wake pia. Mchungaji mwandamizi anahitaji kufundisha mchungaji wa vijana ambaye siyo tu kwamba anawakilisha kanisa tu bali Mungu pia. Unatakiwa kuhakikisha kuwa wanatoa ushauri sahihi kwa vijana na wazazi wanaotafuta msaada. Je! Unaweza kuona jinsi mchakato wa uanafunzi unavyounda mtandao wa uhusiano wa kiroho na umoja ndani ya kanisa, katika uongozi na kati ya kundi? Hivi ndivyo Mungu anavyotaka watoto wake waadilishwe.

Kuna familia nyingi za mzazi mmoja katika jamii, pia kuna vijana wengi walio na wazazi wasio Wakristo. Kuwahudumia watoto hawa ni msingi na lengo kuu kwa huduma ya ushauri kwa vijana, ambayo ni njia nzuri ya kushiriki upendo wa Kristo na mtoto aliye na uhusiano uliovunjika na baba au mama ambaye hayupo, au hakuna ushawishi wa Kikristo nyumbani (James 1:27). Omba na utafute mwongozo wa Bwana kwa kukuza mratibu wa ushauri wa vijana na karama za kiroho na moyo wa kuwafikia watoto hawa. Tembelea tovuti yetu ya www.FDM.world kwa mwongozo wa jinsi ya kuanzisha huduma hii.

**Huduma ya Wanaume au Wanawake**

> Lakini wewe, nena mambo yapasayo mafundisho yenye uzima, ya kwamba wazee wawe wenye kiasi, wastahivu, wenye busara, wazima katika imani, katika upendo na katika saburi na wenye adabu. Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu, wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi; bali wafundishao mema; ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao na kuwapenda watoto wao na kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe ili Neno la Mungu lisitukanwe. Vivyo hivyo, na vijana waume uwaonye kuwa na kiasi, katika mambo yote, ukijionyesha mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema na katika mafundo yako ukionyesha usahihi na ustahivu; na maneno yenye uzima yasiyoweza kuhukumiwa makosa, ili yule mwenye kupinga atahayarike kwa kuwa hana neno baya la kunena juu yetu. (Tito 2: 1-8)

Kifungu hiki cha Maandiko hutoa maono mazuri kwa huduma ya wanaume au wanawake kanisani. Hii ni picha ya wanaume na wanawake Wakristo waliokomaa wanawafundisha waamini wadogo na wasio wakomavu kiroho kuenenda katika haki na kuzingatia mambo ambayo Mungu amewapa kulingana na maagizo yanayopatikana katika Neno lake. Ni wazi kabisa kipaumbele ni kuwafundisha jinsi ya kuelekeza familia kama wenzi na wazazi.

Ni jukumu la mchungaji mwandamizi kuweka vipaumbele kwa kile kinachofundishwa katika huduma zote kanisani, pamoja na huduma ya wanaume na wanawake!

**JIANDAE KUANZA**

*Omba.* Biblia inasema siyo tu kwamba sisi tunapambana na miili yetu lakini tunapambana pia dhidi ya enzi za kiroho na nguvu za giza. Shetani amesababisha upofu, usumbufu, na mkanganyiko katika maeneo haya ya uanafunzi; omba ukweli wa Mungu ushinde katika makanisa na familia zetu, na uinue wanafunzi wengi.

*Wafunze viongozi.* Wachungaji na viongozi, huanza na nyinyi. Wekeni maono na mkakati wa uanafunzi katika makusanyiko yenu. Maagizo juu ya utaratibu wa vipaumbele wa uhusiano wa Mungu, kuelewa maana ya uanafunzi wa kweli na uko kwa ajili ya nani, na kufuata mfano wa Kristo wa uanafunzi kwa kuungana kwa makusudi na watu wote ni sehemu ya mpango mzuri wa uanafunzi. Wafundishe juu ya kukaa ndani ya Kristo yaani, kumfanya awe kipaumbele cha kwanza baada ya wokovu, kifuatiwe na kufundisha ukweli muhimu na wa msingi wa imani ya Kikristo, kutunza ndoa, na malezi, ambavyo ni vipaumbele dhahiri kwa Mungu. Kumbuka, 1 Timotheo 3: 4-5 inasema kwamba wakati nyumba ya kiongozi haipo sawa, huduma yao itakuwa dhaifu.

*Andaa mchungaji au Mlei anayesimamia huduma hiyo.* Uanafunzi ni mapenzi ya Mungu kwa kila muumini lakini, mara nyingi, sisi hatulitendi hili sawasawa. Maono ya kuanzisha kipaumbele cha Kanisa hutoka kwa mchungaji kupitia kuhubiri na kuhimiza kusanyiko; umuhimu wa kufundisha lazima uwasilishwe na mkakati utekelezwe.

*Tunapendekeza sana kutumia vitabu vyetu vya kujifunzia: ambavyo vinapatikana katika* www.discipleshipworkbooks.com, *au matini zilizochapishwa yanapatikana katika <u>www.fdm.world.</u>*

## WITO WA KUCHUKUA HATUA

> Katika yeye mwili wote uliungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo; umejiunga na kuunganishwa pamoja kwa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo. (Waefeso 4:16)

Je! Umeishika hiyo? "Kila sehemu hufanya sehemu yake," kwa hivyo kila mmoja anahitaji kukubali wito huu na kufanya sehemu yake. Ahadi ni kwamba utii huleta baraka na kila muumini anataka kubarikiwa.

Familia zenye nguvu ni muhimu. Tunaona katika sura mbili za kwanza za Biblia kwamba familia ndio taasisi ya kwanza ambayo Mungu aliumba. Agano la Kale na Jipya yote huanza na simulizi za familia. Taifa la Israeli lilikua kutoka kwenye familia moja; katika hali halisi, pendo unatajwa kwa mara ya kwanza unapatikana katika Kitabu cha Mwanzo 22: 2, ambapo tunajifunza juu ya upendo wa Ibrahimu kwa mwanawe. Katika Kumbukumbu la Torati 6: 1-9, Mungu aliweka wazi kuwa kuishi kwa Israeli kama taifa kulihitaji wazazi kuwafundisha na kuwaelimisha watoto wao, ili kuwakuza kulingana na maagizo yake. Mwokozi wetu alikuja ulimwenguni kupitia familia; na muujiza wake wa kwanza liufanya kwenye harusi.

Utakatifu wa ndoa unaonyeshwa katika Waefeso 5:25, wakati Mungu anahimiza mume ampende mkewe kwa namna ile ile ambayo yeye alivyolipenda Kanisa lake kwa kujitoa sadaka. Katika mstari wa 22, Mungu anatoa wito kwa wake kuwathibitisha, kuwaheshimu, na kuwanyenyekea waume zao ili kuuonyesha ulimwengu kile ambacho Mungu anataka kutoka kwa watakatifu wake. Hii ni mifano michache tu inayoonyesha umuhimu ambao Mungu huweka kwenye taasisi ya familia. Na, ikiwa familia ni kipaumbele kwa Mungu, basi inapaswa pia kuwa kipaumbele kwa Kanisa.

Kwa miaka mingi, Makanisa yameendelea katika huduma kwa watoto na vijana kwa kutenda zaidi ya kuwa na "shule ya Jumapili" na kuajiri wachungaji wa vijana ili kukuza vikundi na shughuli. Ni wazi kwamba Makanisa yamefanya vijana kuwa kipaumbele; Lakini, wengi wamefanya kwa kiasi kidogo ambapo lengo limekuwa kufundisha na kuelekeza ndoa na wazazi wanaounda familia za watoto hao. Mkazo zaidi unatakiwa kuwekwa kwa waume, wake, na uzazi kama tunavyofanya kwa vijana, na tutaona mabadiliko ya kweli katika familia na muundo wa Kanisa. Takwimu zinaonyesha kuwa watoto waliolelewa kulingana na kanuni za Ki Biblia kwa kuwa na wazazi ambao huakisi mfano wa Kristo katika maisha yao wenyewe wana uwezekano mkubwa wa kuishi ndani ya Kristo hata baada ya kutoka kwenye familia zao.

Biblia ni mwongozo bora zaidi uliowahi kuandikwa kuhusu ndoa na malezi, lakini maagizo yake yameenea kote. Tunapoandaa mada fulani ya kusoma na kuelekeza watu, ni vizuri

sana kuwa na vitabu hivi vya kujifunzia. Mpangilio wa kanuni, amri na maswali kadhaa ya mwongozo vinaweza kuleta mafanikio makubwa katika mchakato wa kuwafundisha watu ndani ya Kanisa. Wakristo ambao wamepewa matini hizi na wamepata muda wa kuzifanyia kazi katika maisha yao, wanaweza kufanikiwa zaidi kuandaa wanafunzi wengine kuwasaidia kutatua masuala ya malezi. Hii ndio namna tunayoweza kuona familia zikimjua na kumtukuza Mungu. Kanisa linahitaji maono mapya ya uanafunzi na vipaumbele vilivyo wazi ikiwa kweli tunataka kubadilisha mwelekeo wa uharibifu wa familia nyingi za Kikristo.

Jiulize maswali haya ya kutafakari:

- Kwa nini Wakristo wengi hawaelewi maana ya kuwa mwanafunzi, au ni jinsi gani mtu hutenda ili kuwa mwanafunzi?
- Kwa nini Wakristo wengi hawayatendi yale mambo ya upendeleo muhimu zaidi waliyopokea pamoja na wokovu, nafasi ya kuwa na Yesu kila siku katika kujifunza na kuomba (ibada)?
- Kwa nini Wakristo wengi hawajui ukweli kwamba kukaa ndani ya Kristo kila siku ni namna pekee ambayo tunapokea nguvu ya kumtii?
- Kwa nini familia nyingi za Kikristo zinaumia na zina matatizo?
- Je! Kanisa limepunguza viwango vinavyoihusisha familia bora?
- Je! Kanisa linafanikiwa wakati Wakristo wengi hawajui jinsi ya kukaa ndani ya Kristo kila siku na familia zao ziko nje ya mapenzi ya Mungu na zinaangamia?
- Je! Kanisa linafanikiwa wakati asilimia kubwa ya watu wake hawajui muundo na maagizo ya Mungu ya kuwa mwanafunzi, mume, mke, na mzazi?
- Je! Makanisa yanatambua kwamba kuleta wongofu ni kazi ya Roho Mtakatifu, na uanafunzi ni mpango wa Mungu ulioandaliwa ili kuwatambua watu wake, jambo ambalo ni kazi yetu?

- Je! Kusudi kuu la Kanisa ni kuwezesha ukuaji wa kiroho -uanafunzi?

Sote tunaweza kukubaliana kwamba lengo la uinjilisti ni wokovu katika Yesu Kristo. Tunaweza pia kukubaliana kwamba huu ni mwanzo tu wa maisha ambayo Maandiko yanahitaji "kukaa ndani ya Kristo" (Yohana 15: 1-8). Huu ndio mtindo wa maisha ya mwanafunzi wa Kristo; lakini kama ambavyo kueneza Injili kunahitaji juhudi za kibinadamu, ndivyo hivyo pia kwa mchakato wa ukuaji wa Kikristo. Hapa ndipo kufundisha kunakuwa muhimu na ni jukumu tulilopewa na Yesu katika Agizo Lake Kuu. Uanafunzi ni mchakato wenye lengo; unaohusisha uhusiano binafsi kati ya waamini ambao wanahimizana kuingia katika uhusiano wa karibu, wa kudumu na Yesu Kristo, kukua katika ukomavu wa kiroho na kujifunza jinsi ya kutenda mambo ambavyo Mungu ametupatia katika Neno lake. Haya hujumuisha mafundisho, maelekezo, sala, kutiwa moyo, uwajibikaji, kukaripia, kusahihisha, kutoa muda, na kujituma.

Yesu anatutaka tueneze Injili na kufanya watu kuwa wanafunzi. Uinjilisti wenye nguvu na ufanisi zaidi utaonekana wakati Wakristo wanapokaa ndani ya Kristo na kufuata Neno la Mungu kwa kutii mapenzi yake. Hapo ndipo maisha yetu yatakapoakisi na kumtukuza Mungu wa kweli aliye hai kwa ulimwengu wenye giza na unaoangamia. Ni maombi yangu kwamba habari hii juu ya uanafunzi itawahamasisha kama Kanisa, kuleta upya au maono mapya na kwamba Bwana atainua wanafunzi wengi kuambatana pamoja na wengine walio tayari kufundisha, kutia moyo na kuonyesha mfano wa maisha ya kukaa ndani ya Yesu na Neno lake.

Ni maombi yangu kwamba habari hii imekubariki na kukutia moyo. Tafadhali tujulishe ikiwa tunaweza kusaidia kuanzisha huduma endelevu ya uanafunzi katika Kanisa lako. Matini zetu zinatumika ulimwenguni kote na kwa sasa tunazo nyingi ziliyotafsiriwa kwa Kihispania, Kirusi, na Kichina. Mungu anawabariki watu ulimwenguni kote kupitia ukweli uliomo katika vitabu vyetu vya kujifunzia. Tunaendelea kufikia nchi nyingine mpya kwa kufanya mikutano na kuyasaidia makanisa kuanza kujumuisha muundo wa uanafunzi katika makanisa yao.

Bwana awabariki, abariki familia zenu, na huduma zenu katika Kristo,
Mch. Craig Caster, mwanzilishi wa FDM.

## KUHUSU MWANDISHI

Mtu mjinga, mwanafunzi mwenye uwezo duni wa kujua kusoma na kuandika. Mwanafunzi aliyehitimu kitado cha sita kwa ufaulu wa daraja la tatu. Mume mjinga na baba mnyanyasaji. Yote hayo yanauelezea Mch. Craig katika kipindi fulani maishani mwake; lakini Mungu alikuwa na mpango tofauti kabisa kwa ajili ya maisha yake. Pamoja na Mch. Craig kuwa mwoga kuzungumza mbele za watu, Mungu alimuita kuwa mtumishi wa kudumu mwaka 1994. Aliingia katika Imani bila elimu maalum ama shahada ya seminari. Aliteuliwa mwaka 1995, na toka hapo ameandika vitabu vinne; amefundisha wanaume wengi, ameshauri mamia, wamewaleta kwa Yesu wengi wasiohesabika na kuwafundisha maelfu kupitia semina za ndoa na malezi. Ametoa pia mafunzo ya wanume na semina za Wachungaji kwa taifa la Marekani na kimataifa. Amefanya yote hayo kwa Neema ya Mungu.

Pamoja na kwamba Craig alipa Yesu maisha yake mwaka 1979, kuongoka kwake kulianza pale alipoanza kutenda kila siku kadiri ya maagizo ya Yesu na Neno lake. Aliamini kwa dhati kwamba Yesu anatamni uhusiano kwa karibu na kila mmoja wetu. Maisha yake yalibadilika kwa sababu aliutafuta uhusiano huo na Yesu na akamtegemea katika kila jambo.

### Tiwa moyo

Kama unapambana kuamini kuwa Mungu anaweza kutenda ndani yako na katika maisha yako yote, basin a utiwe moyo kutokana na simulizi la Mch, Craig. Usiruhusu dhambi zako za zamani, uwezo wako mdogo, woga wa kuzungumza na kukosa elimu vikufanye wewe kutokutii wito wa Mungu katika maisha yako. Mungu anataka kukufanya mwanafunzi wake, na kama umeoa au kuolewa au una watoto, basi anataka kukufanya uwe mwenza na mzazi unayemtukuza yeye. Neema zake ni za ajabu na hazina mipaka. Anakupenda na anashauku ya kutukuzwa kupia wewe.

### Ahadi ya Mungu kwako

Na ashukuriwe Mungu kwa ahadi zake nyingi na kutuhudumia; tafakari zaidi ahadi zake kutoka kwa Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristu; kwa wale waliopata Imani moja na sisi, yenye thamani katika haki ya Mungu wetu na mwokozi wetu Kristo. Neema

na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu. Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utaua, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washiriki wa tabia za Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliyomo duniani kwa sababu ya tamaa. Naam na kwa sababu hiyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu katika imani yenu tieni na wema; na katika wema wenu, maarifa na katika maarifa yenu, kiasi na katika kiasi chenu saburi na katika saburi yenu utauwa na katika utauwa wenu, upendano wa ndugu na katika upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo.

## KUHUSU HUDUMA YA UANAFUNZI KATIKA FAMILIA

Huduma ya uanafunzi katika familia (FDM), ni shirika lisilo na kibiashara lililoanzishwa mwaka 1994 chini ya mwanzilishi na Mkurugenzi Mch, Craig Caster, kwa lengo la kusaidia, kufundisha na kuelimisha muundo wa kanisa la Kristo kuendesha familia kwa njia ya uananfunzi. Ili kilifanikisha hili, FDM hutoa vitabu vya kujifunzia, video zinazohusiana na mafunzo na matini za mtandaoni kwa ajili ya masomo binafsi, vikundi vidogo vidogo, vikundi ya mafunzo kwenye familia, na mwanafunzi mmoja mmoja. Hutoa semina kuhusu uanafunzi, ndoa na malezi.

Lengo kuu la FDM ni kufundisha na kusaidia viongozi wa Makanisa ya Kikristo kuanzisha maono ya uanafunzi na kuipatia jamii matini za kujifunzia ili kuwasaidia kuendesha familia na makanisa yao. Toka mwaka 1995, maelfu ya watu wamehitumu masomo ya ndoa na malezi, mamia ya Makanisa ya Marekani na mataifa mengine pia wamekuwa wakitoa huduma kwa waumini wao kupitia matini hizi. Huduma zao pia zimesaidia watu wengi kupitia mafunzo ya bure yanayopatikana kwenye www.FDM.world.

FDM inahudumu zaidi kimataifa katika nchi kama Urusi, Ukrain, Cuba, Mexiko, Afrika, Singapo, Japan na China. Pata mambo mengine zaidi kwenye tofuti yetu www.FDM.world.